

Sheria Ndogo za Halmashauri Manispaa ya Tabora (Usafi wa Mazingira)
Tangazo la Serikali Na.361

Tangazo la Serikali Na. 361 la tarehe 4/9/2015

..
SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

**SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI MANISPAA YA TABORA (USAIFI
WA MAZINGIRA) YA MWAKA 2014**

SEHEMU YA KWANZA:
UTANGULIZI

Jina 1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora (Usafi wa Mazingira), 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la Matumizi 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo;

“Nyumba ya kuishi” maana yake ni jengo la mtu binafsi au la Umma linalotumika na lisilotumika kwa ajili ya makazi ya binadamu.

“Mamlaka” maana yake ni mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

“Afya” maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na sio tu kuwa na ugonjwa au ulemavu.

“Afisa Afya” maana yake ni Afisa afya aliyeajiriwa na Halmashauri.

“Afisa Afya Msaidizi” maana yake ni msaidizi wa Afya aliyeajiriwa na Halmashauri.

“Chukizo la Afya” maana yake ni kitu chochote kinachoweza kuleta madhara au kuhatarisha afya ya binadamu.

“Jengo la Biashara” maana yake ni jengo lolote lilijengwa na kuidhinishwa na mamlaka kufanya biashara iliyokusudiwa.

“Usafi wa Mazingira” unatafsiriwa kama hali ya kupambana na njia zote katika mazingira ya binadamu ambazo zinaleta au zinaweza kuleta madhara kimaendeleo, kiafya na kimaisha.

“Mazingira” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira 2004 yanahusisha maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za Kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jisi yanavyoingiliana.

“Usafi” Ni kuondoa taka ngumu, maji, taka, kuondoa kinyesi au mizoga yeche harufu mbaya.

“Takataka” maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

“Choo” maana yake ni eneo linalotumika kuhifadhi kinyesi cha binadamu kinaweza kuwa cha:

- (i) Shimo lililochimbwa lisilopungua kina cha futi nane, lililojengewa banda imara limeezekwa na kusakafawa, lina mlango na mfuniko wa tundu.
- (ii) Kutumia maji kilichoengewa sahani ya udongo wa China iliyounganishwa kwenye mfereji/bomba linalopitisha kinyesi kuelekea kwenye mabwawa ya kusafisha/kutibu maji taka au shimo lililochimbwa chini ya ardhi siyo chini ya mita 3.0 na upana wa mita 1.

SEHEMU YA PILI USAIFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa
kutunza
Usafi wa
Mazingira

4. Niwajibu wa kila mmiliki au mpangaji au mkazi wa Halmashauri ya manispaa ya Tabora:-

- (a) kuwa na nyumba yenyе kujengwa kwa kuta imara,kuezekwa na kuwa na madirisha ya kutosha kuingiza hewa na mwanga wa kutosha;
 - (b) kuhakikisha kuwa nyumba yake ina choo imara na bora,chenye shimo refu lisilopungua futi nane (8) chenye jengo imara,paa,milango,mfuniko wa tundu kwa ajili ya kuzuia au kutoa wadudu kama inzi,mende,n.k na kuhakikisha kuwa choo hicho kinatumika wakati wote.
 - (c) kuwa na kichanja cha kuanikia vyombo chenye kimo kisichopungua futi nne (4) toka usawa wa ardhi.
 - (d) kuwa na shimo la kutupa takataka au chombo imara chenye mfuniko kabla ya kupeleka kwenye shimo na kuhakikisha kuwa takataka zinachomwa moto na shimo linapojaa linafunikwa.
 - (e) kusafisha maeneo yanayozunguka nyumba yake na kuyaweka katika hali ya usafi kwa kuondoa takataka zote, kulima majani,kufagia,kuondoa na kuharibu mabaki ya makopo,vyungu,vibuyu na vitu vyote vinavyoweza kuhifadhi maji na kusababisha mazalia ya wadudu wanoweza kuathiri afya yake kama vile mbu.
 - (f) Atalazimika kusafisha, kufukua mfereji wa maji ya mvua uliopita mbele au au nyuma,kushoto au kulia kwa nyumba yake.
 - (g) kufukia au kukausha madimbwi yote yanayotunza maji kuzunguka eneo la nyumba yake.
 - (h) Atalazimika kuwa mdau na atawajibika kutunza na kuendeleza mazingira na kutoa taarifa kwa Mamlaka husika kuhusu shughuli au jambo lolote ambalo kwa kiasi kikubwa linaweza kuathiri au linaathiri afya za binadamu au mazingira na faini itakayolipwa na mtuhumiwa, mkamataji atapewa asilimia 20.
- 5.-(1) Endapo katika ukaguzi wa Afya itagundulika mtu ye yeyote amekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi Afisa Afya atatoa notisi ya siku saba (7) kwa mwenye nyumba na iwapo hapatikani notisi hiyo itatolewa kwa Mpangaji au Wapangaji ikieleza masharti ya kufanya ili kurekebisha hali hiyo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (1) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba hiyo isitumike kwa shughuli za makazi hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.

6.-(1) Itakuwa ni wajibu wa Kila mmiliki wa kiwanda, gereji, mahali pa ujenzi au mahali popote walipoajiriwa zaidi ya watu wawili, shule, baa, kilabu, mgahawa, hoteli,nyumba ya kulala wageni, nyumba ya cinema au nyumba yoyote inayotumika kwa starehe au shughuli ya jamii, kuhakikisha kwamba anaweka na kutunza vyoo vya kutosha kwa matumizi tofauti ya wanaume na wanawake. Vyoo hivyo pia vizingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yeyote awe mwenye nyumba au mpangaji kutupa taka barabarani,uchochoroni, nje ya pipa la taka,sokoni,maeneo ya huduma za jamii,maeneo ya wazi au sehemu iliyotengwa kuhifadhi taka hadi zitakapozolewa.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yeyote:-

- (a) kufanya matengenezo makubwa ya magari au pikipiki nyumbani au barabarani (gereji za mitaani)
- (b) kuegesha au kutelekeza gari bovu au sehemu ya gari bovu barabarani.
- (c) kufanya biashara ya pombe ya aina yoyote katika nyumba ya kuishi;
- (d) kuuza matunda na bidhaa zingine za vyakula barabarani bila ridhaa ya Halmashauri;
- (e) kufanya mikusanyiko wakati wa mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza bila idhini ya Halmashauri;
- (f) kuchimba na kufyatua tofali kandokando ya barabara,maeneo ya wazi,au maeneo yaliyotengwa kwa shughuli maalumu.
- (g) kuchimba mchanga kandokando ya barabara,maeneo ya wazi,au maeneo yaliyotengwa kwa shughuli maalumu;
- (i) kuuza vyakula vilivyoharibika au visivyofaa kuliwa na binadamu.

- (j) Kupanda mazao yenyе urefu wa kuzidi sentimita 30 katika kata ya Cheyo, Ipuli, Tambukareli, kiloleni, Isevy, kanyenye, Kitete, Mbugani, Ng'ambo, Gongoni na Chemchem.

SEHEMU YA TATU
UHIFADHI WA VYANZO VYA MAJI

Wajibu
Wa
Halmashauri
Kulinda
Vyanzo
Vya maji

Kulinda
Eneo la
hifadhi

7-(1) Halmashauri itawajibika kuanzisha ,kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu ye yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

8-(1) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakua ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelezo ya Afisa Mistu.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kumiliki eneo la chanzo cha Maji isipokuwa Halmashauri.

9-(1) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote,Kiwanda,Taasisi,Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito,mabwawa,ziwa,visima,mifereji,chemichemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(2) Ni marufuku mtu ye yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kwenda haja kubwa au ndogo kwenye au karibu na mto.

(4) Ni marufuku kwa mwenye kiwanda,gereji,stesheni ya umeme au shughuli nyingine yoyote ile,kufanya kitendo chochote cha kuchafua maji ya mto au kisima yanayotumika kwa kunywa au matumizi mengine ya nyumbani.

Sheria Ndogo za Halmashauri Manispaa ya Tabora (Usafi wa Mazingira)
Tangazo la Serikali Na.361

Adhabu 10. Ni marufuku kuoga,kufua,kuosha vyombo au kucheza katika eneo la bomba la maji ya uma. 10. Mtu ye yote atakaevunja au kwenda kinyume na kifungu chochote cha sheria hizi atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini za kitanzania (50,000/=) papo kwa papo palipotokea tendo la kuvunja Sheria na endapo atashindwa kutoa faini hiyo atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu mia moja za kitanzania (100,000/=) au kutumikia kifungo cha miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA
TOZO ZA UCHANGIAJI USAFI WA MJII

Na.	VYANZO VYA MAPATO	KIWANGO KWA MWEZI	KIWANGO KWA MWAKA
1.	Kaya moja	1,000.00	12,000.00
2.	Duka la rejareja kata za mjini	3,000.00	36,000.00
3.	Duka la rejareja kata za nje ya mjini	1,000.00	12,000.00
4.	Mashine ya kukamua mafuta ya alizeti	4,000.00	48,000.00
5.	Duka la jumla	10,000.00	120,000.00
6.	Gereji	5,000.00	60,000.00
7.	Migahawa	5,000.00	60,000.00
8.	Mashine za kukoboa mpunga	5,000.00	60,000.00
9.	Vilabu vya pombe	4,000.00	48,000.00
10	Mama lishe/Baba lishe	2,000.00	24,000.00
11	Viwanda vya uselemala	10,000.00	120,000.00
12	Mashine za mbaao	7,000.00	84,000.00
13	Bucha	4,000.00	48,000.00
14	Nyumba za kulala wageni	4,000.00	48,000.00
15	Saloon/kunyoa nywele	3,000.00	36,000.00
16	Mashine za kukoboa na kusaga nafaka	5,000.00	60,000.00
17	Godown	12,500.00	150,000.00
18	Petrol station	5,000.00	60,000.00
19	Grocery/Bar	4,000.00	48,000.00
20	Hotel	12,500.00	150,000.00
21	Biashara ya chips	4,000.00	48,000.00
22	Wauza Mkaa jumla	5,000.00	60,000.00
23	Mafundi kushona nguo	3,000.00	36,000.00

Sheria Ndogo za Halmashauri Manispaa ya Tabora (Usafi wa Mazingira)
Tangazo la Serikali Na.361

Na.	VYANZO VYA MAPATO	KIWANGO KWA MWEZI	KIWANGO KWA MWAKA
24	Biashara ya samaki wabichi	4,000.00	48,000.00
25	Mafundi vyuma(wahunzi)	5,000.00	60,000.00
26	Kumbi za starehe	5, 000.00	60,000.00
27	Nyumba za cinema	4,000.00	48,000.00
28	Majengo ya kuoshea magari/pikipiki	5,000.00	60,000.00
29	Viwanda vya aina zote	17,000.00	204,000.00
30	Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGo)	5,000.00	60,000.00
31	Shule za misngi binafsi	17,000.00	204,000.00
32	Shule za sekondari	17,000.00	204,000.00
33	Nyumba za kulala wageni/bar	10,000.00	120,000.00
34	Nyumba za kulala wageni na zenye mgahawa	5,000.00	60,000.00
35	Ukaguzi wa jengo jipya		20,000.00
36	Bakery	10,000.00	120,000.00
37	Stationery	2,500.00	30,000.00
38	Taasisi za serikali	17,000.00	204,000.00
39	Makampuni Binafsi	17,000.00	204,000.00
40	Pharmacy	5,000.000	60,000.00
41	Maduka ya dawa muhimu kata za mjini	3,000.00	36,000.00
42	Maduka ya dawa muhimu kata za nje ya mjini	1,000.00	12,000.00
43	Uchunguzi wa ramani		20,000.00
44	Wauzaji wa samaki	3,000.00	36,000.00
45	Hospital watu binafsi	10,000.00	120,000.00
46	Kituo cha Afya/Zahanati	5000.00	60,000.00
47	Maabara binafsi	5000.00	60,000.00
	Meza sokoni	2000.00	24,000.00
48	Kutupa taka dampo Halmashauri	10.000 @ tones	
49	Fundi baiskeli	1,000.00	12,000.00
50	Fundi pikipiki	3,000.00	36,000.00
51	Wafanyabiashara ndogondogo	1,000.000	12,000.00
52	Maduka ya M- Pesa, Tigo n.k.	2,000.000	24,000.00

Sheria Ndogo za Halmashauri Manispaa ya Tabora (Usafi wa Mazingira)
Tangazo la Serikali Na.361

Na.	VYANZO VYA MAPATO	KIWANGO KWA MWEZI	KIWANGO KWA MWAKA
53	Kupulizia (fumigation)	5,000.000	60,000.00
54	Usajili baraza la Afya mazingira Taifa		50,000.00

JEDWALI LA PILI
BIASHARA NDOGONDODO

Na.	VYANZO VYA MAPATO	KIWANGO KWA MWEZI	KIWANGO KWA MWAKA
1	Biashara ya matunda	2,000.00	24,000.00
2	Biashara ya miwa	3,000.00	36,000.00
3	Biashara ya urembo	1,000.00	12,000.00
4	Biashara ya shoes shine	1,000.00	12,000.00

JEDWALI LA TATU
BIASHARA YA MITUMBA

Na.	VYANZO VYA MAPATO	KIWANGO KWA MWEZI	KIWANGO KWA MWAKA
1	Biashara ya nguo	3,000.00	36,000.00
2	Biashara ya viatu	3,000.00	36,000.00

SEHEMU YA TANO.
TOZO YA UONDOAJI MAJI TAKA

Na.	VYANZO VYA MAPATO	KIWANGO KWA TRIPU	KIWANGO
1	Nyumba watu binafsi	Tripu 1	50,000.00
2	Wafanyabiashara/Taasisi	Tripu 1	40,000.00